MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 10 TOLEO 40

MEI 29, 2009

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!

UCHAGUZI MDOGO BUSANDA

CCM YATAMALAKI!

CHADEMA YAANGUKA KIUME

Na. M. M. Mwanakijiji

Chama cha Mapinduzi kimeendelea kuonesha kuwa kinaweza kuhimili kuzomewa, kuchafuliwa na kurushiwa kila aina ya tuhuma na kuibuka kidedea katika chaguzi mbalimbali nchini. Tangu wimbi la mahubiri ya kashfa mbalimbali kuanza kukiandama kwa kasi kubwa kuanzia 2005 na baadhi ya viongozi wake kujikuta wakigubikwa na kashfa nzito za mabilioni ya shilingi na wengine kusimamishwa kizimbani Chama cha mapinduzi kimeonekana ni kisiki kizito kuking'oa madarakani.



Mbunge mpya wa Busanda, Bi.

Hilo limethibitika tena Jumamosi na Jumapili iliyopita ambapo CCM imeweza kuibuka mshindi katika chaguzi mbili ndogo za Magogoni huko Zanzibar na ile ya Busanda, Geita huko Mwanza. Hata hivyo uchaguzi uliokuwa una mvuto wa aina yake ni ule wa Busanda ambapo kwa mara ya kwanza CCM ilikabiliwana upinzani mzito kutoka kwenye Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) ambacho wachunguzi wengi wa siasa za ndani (nikiwemo mimi) tuliamini kuwa kina uwezo na sababu za kisiasa za kushinda uchaguzi huo.

Hata hivyo, jinsi CCM ilivyokuwa imepania kutokupoteza jimbo hilo na jinsi tofauti ya kura kati yake na Chadema vimetoa shaka yoyote kuhusu CCM kuwa ni chama chenye mvuto kwa mashabiki



Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Ijumaa**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Chapa nakala angalau moja na umpatie mtu asiye na mtandao bure!**

Ndani ya Toleo Hili

CCM Yatamalaki	1,2
Mwakyembe aja juu	1, 4
CCM yatamalaki Busanda	3
Dajessy: Suala la Ndoa -2	4
Riwaya ya Mwanakijiji	5
Hoja: Tususie mafisadi?	5
Picha, Katuni na Maoni	6

POLISI NI WAPIGA RAMLI?—MWAKYEMBE

Na. Rashid Mahmoud

Mbunge wa Kyela Dr. Harrison Mwakyembe amesema kuwa taarifa iliyotolewa na kamati ya Polisi iliyoundwa kuchunguza chanzo cha ajali iliyomkuta wiki iliyopita imejaa taarifa zisizo na msingi katika ukweli na ya kuwa imemuacha akiwa na maswali mengi zaidi sasa hivi juu ya ajali hiyo kutokana na jinsi ambavyo Jeshi la Polisi limeshughulikia suala hilo tangu apate ajali.

Katika taarifa yake kwa waandishi wa habari iliyotolewa jana, Dr. Mwakyembe ameeleezea kusikitishwa kwake na taarifa hiyo iliyotolewa na Kamanda wa Vikosi vya Usalama barabarani nchini Bw. James Kombe. Dr. Mwakyembe amesema kuwa "Taarifa hiyo ya Polisi inakanusha maelezo yangu yote na ya dereva wangu kuhusu ajali ilivyotokea na kunitaka nijiepushe kutoa matamshi kuhu-

USHINDI WA CCM BUSANDA

wake, chenye mkakati mzuri wa kisiasa na ambacho kiko tayari wakati wowote ule kutumia raslimali zake na za nchi kujihakikishia ushindi "by any means necessary". Hata hivyo, siamini kuwa ushindi wa Busanda ulitokana na mchezo wowote mchafu bali mahesabu ya kisiasa ya wanamkakati wa CCM ambao wengi wao ni wataalamu katika propaganda za kisiasa na wazoefu wa muda mrefu wa chaguzi mbalimbali nchini.

Hivyo, ni katika kulielewa hilo sina budi kukubali kuwa ile "ishara kutoka Magharibi" ambayo niliizungumzia licha ya kuwa ipo na imetokea kule Busanda ukweli unabakia kuwa mwanga wake umefichwa na ushindi wa kishindo kama cha Tsunami wa chama tawala.

Na katika hilo demokrasia ya kweli inatuita tutoe mkono wa pongezi na heri kwa Mbunge mpya wa Busanda na kwa wanaharakati wa Chama cha Mapinduzi, makada na wapambe wake wote kwa ushindi huo ambao ninaamini kama ule mwingine wa Mbeya Vijijini, Kiteto au Tunduru umeendelea kutoa somo ambalo hatuna budi kulitafakari katika makala hii.

Somo la pande mbili

Ninaamini ushindi wa CCM Busanda unatuacha na pande mbili za somo kubwa. Upande wa kwanza ni somo kwa wapinzani kuelewa ni jinsi gani CCM inashinda chaguzi hizi ndogondogo na kwa kiasi kikubwa uchaguzi mkuu na upande wa pili ni somo kwa CCM kuelewa kuwa wapiga kura wameanza kubadilika. Naomba nianze na hilo la pili kwa kifupi ili niweze kuzungumzia hilo la kwanza kwa kirefu.

Wapiga kura wanabadilika.

Katika makala yake kwenye Daily News Makamu Mwenyekiti wa CCM (Bara) Bw. Pius Msekwa alielezea ni jinsi gani CCM waliweza kushinda kule Kiteto na mkakati waliotumia. Maelezo yake (ambayo nimeyasoma siku chache tu zilizopita nikijiandaa na makala hii) yanakubaliana na mtazamo wangu wa kwanza kuhusu ushindi wa CCM Busanda.

Mhe. Msekwa ambaye amewahi kuwa Mbunge wa muda mrefu, na Spika wa Bunge la Muungano ameeleza kuwa Chama chake kiliangalia mkakati wa wapinzani na kuamua kuchukua mkakati ambao ulitegemea zaidi wanachama wake kuliko wapiga kura wapya au watu wasio na chama cha kisiasa.

Kimsingi mkakati huo ndio pia umetumika Busanda ingawa ulipojaribu kutumiwa kule Tarime ulishindwa kutokana na ukweli kuwa hata Chadema walitegemea nguvu ya wanachama wake ambao walikuwa ni wengi na waliohamasika zaidi.

Mkakati huu hata hivyo una kikomo chake kama tulivyoona Busanda. Kulinganisha matokeo ya uchaguzi wa Wabunge 2005 na huu mdogo utaona kuwa CCM imeshinda safari hii kwa kura chache zaidi wakati Chadema kimepata kura mpya kwa karibu asilimia 40 kulinganisha na mwaka 2005 ambapo kilipata asilimia 4 tu!

CCM haiwezi kuendelea kutegemea nguvu ya wanachama wake tu ni lazima ivutie watu nje ya chama na ambao wana mlengo wa mabadiliko ya kweli. Tukiangalia kura za Busanda tunaweza kuona pasipo shaka yoyote kuwa japo ni kweli kabisa CCM imeshinda uchaguzi lakini ukweli mkubwa zaidi ni kuwa Chadema imeshinda mioyo ya wananchi wa Busanda.

Haiwezekani kuelezea kwa chama kichanga kama Chadema kuweza kuzoa zaidi ya kura elfu 20 wakati miaka kama minne tu ilipata kura zisizodizi 4000! Na kwa vile tunatambua kuwa wapiga kura wengi zaidi hawakupiga kura (karibu 80,000) ni wazi kuwa kama nusu tu yao wangepiga kura na kiwango cha ongezeko la kura kingebakia kama kilivyokuwa Chadema ingeibuka na ushindi wa kushtua.

Kwa hiyo, ninaamini CCM wanaangalia kwa karibu huku kubadilika kwa aina mbili kwa wapiga kura, kwanza wapiga kura wengi hawajitokezi (hili lilitokea Kiteto vile-vile) na pili kati ya wale wanaojitokeza wengi wanapigia kura upinzani kuliko miaka ya nyuma. Somo hili CCM haina budi kutafakari kama inataka kuendelea kushinda kwani kama Chadema itaendelea na wimbi lake la kupata kura mpya namna hiyo ni wazi kuwa mwakani kuna makubwa ya kushuhudia.

Siri ya ushindi wa CCM

Nikirudi kwenye upande wa kwanza wa somo la Busanda naweza kusema pasipo shaka kuwa CCM imeshinda kutokana na muunganiko wa mambo kadhaa ambayo yameathiri upinzani, hilo la umoja lisipokuwa mojawapo.

Kuhubiri tu ufisadi hakuleti ushindi.

Kuanzia wakati wa kashfa ya Buzwagi hadi hivi sasa wapinzani wamekuwa wakihubiri juu ya maovu ya CCM na katika majukwaa yao wamekuwa wakiorodhesha mafisadi mbalimbali. Katika hili wamejijengea jina kubwa sana katika vita dhidi ya ufisadi. Kwanini mahubiri hayo hayaleti ushindi hata kwenye majimbo yaliyo karibu na mijini kama lile la Mbeya Vijijini?

Jibu langu ni kuwa, kuutangaza uovu peke yake au kwa msisitizo mno hakuwafanyi watu waukimbilie wema. Wanatheolojia na wataalamu wa maadili na miiko wanadokeza tangu enzi na enzi kuwa ukiupinga sana uovu bila kuutangaza sana wema basi utaonekana kama unatukuzwa na matokeo yake watu wanazidi kuufanya uovu huo. Ni kwa sababu hiyo utaona wahubiri wazuri siyo wale wanaotishia watu kwenda Jehanamu kutokana na "madhambi" yao bali wale wenye kuvutia mahubiri ya mbinguni na uzuri wa kutenda mema.

Kwa miaka hii miwili au zaidi mahubiri dhidi ya ufisadi japo yanastahili na ya kupongezwa ni lazima yafike mahali yageuka kueleka uzuri wa kufuata mema, kuheshimu sheria n.k Mifano ya watu waliotenda vizuri katika kazi zao, waliokataa rushwa na waliotetea raslimali zetu ni michache mno au haijulikani. Matokeo yake wapiga kura wanakuwa ni kama wamepigwa ganzi kwani hakuna jipya.

Ni kwa sababu hiyo, wapinzani hawana budi kuhubiri ni yapi mazuri ambayo wao watafanya kulinganisha na CCM na kuyasisitiza hayo bila kupuuzia ufisadi. Lengo likiwa kuonesha kuwa wema unalipa vile vile. Mifano ya wale wanaoitwa "mafisadi" kwa kweli ukiangalia utaona ni wale mabilionea na wafanyabishara wakubwa na watu ambao kijamii wanaonekana "wamefanikiwa". Je hawa wanamfanya vipi mtu mwingine kuuchukia ufisadi?

Siasa za kitaifa siyo za mahali

Mojawapo ya hotuba zilizosisimua watu wengi ni ile ya Zitto kule Katoro ambapo alielezea kwa kirefu kwa wananchi wa Busanda ni nini maana ya kuipigia kura

KARIBU MWANAKIJIJI.COM

CCM YATOA SOMO BUSANDA!

CCM (tuliitoa sehemu yake kwenye kijarida kilichopita). Nikiangalia nyuma naweza kusema kuwa hotuba ile ilitakiwa kuwa ni ya kugombea Urais au ya kutolewa kitaifa na siyo ya mahali.

Kwa wananchi wa Busanda mambo ya kitaifa yanawagusa lakini kwao kuna mambo ya mahali (local issues) ambayo yanawagusa zaidi. CCM inalitambua hili na ndiyo maana katika mahubiri yake iliendelea na ahadi za umeme, maji n.k Wakati mgombea wa upinzani anaahidi vitu hivyo yule wa CCM akiahidi watu wanasikiliza zaidi kwa sababu nyuma yake yupo Waziri Nishati na Madini! Wakizungumzia mambo ya shule, nyuma yupo kiongozi wa serikali anayehusika na mambo ya elimu.

Hivyo, jukumu kubwa zaidi ni kwa upinzani kuweza kuzielewa siasa za mahali na mambo yanayowatatiza na hayo ndiyo ya kuahidi kuyafanyia kazi. Yale ya kitaifa ni kama nyongeza tu lakini mwananchi wa jimbo fulani anataka kuona matatizo yake ya pale (immediate problems) ndiyo yanashughulikiwa.

Hivyo, siyo wakati wote mahubiri juu ya EPA, Meremeta n.k yanawagusa watu wa kijijini. Wengi yawezekana hawajapata nafasi ya kufuatilia kwa undani mjadala mzima wa kiuchumi na matokeo yake. Wengi labda wanasikia zaidi radioni na wale ambao wanaweza kusoma kuweza kusoma kwenye magazeti mbalimbali. Vinginevyo, mtu wa kawaida (awe mjini au kijijini) kinachomgusa zaidi ni kile cha mazingira yake hayo ya Minara ya benki kuu, au mambo Deep Green Finance na tarehe za wizi huo bado hayamfikia.

Ni kwa sababu hiyo basi mtu atakayehubiri juu ya shule ya msingi Katoro na yule atakayehubiri juu ya fedha za Chenge Isle of Man huko Uingereza ni wazi yule wa Katoro atakuwa na mvuto wa kupatiwa kura wakati yule mwingine atakuwa na mvuto wa kuhabarisha tu.

CCM inakuja ikiwa na makali kuwili

Mojawapo ya vitu ambavyo tumevishuhudia mara nyingi na sijui ni jinsi gani tunaweza kuviangalia ni jinsi gani viongozi wa serikali ambao pia ni viongozi wa chama wanashiriki kampeni. Unapokuwa na Waziri wa serikali ambaye ni Mbunge na mkazi wa wa maeneo ya uchaguzi na anakuja kama mwanasiasa na kutoa ahadi za serikali wapinzani wajibu vipi hapo?

Fikiria Waziri Ngeleja kwa mfano na Waziri Magufuli; hawa wanakuja kama wabunge au mawaziri? NI wazi haiwezekani kutenganisha sehemu hizo mbili na hivyo kumfanya mwananchi wa kawaida kushindwa kujua anayemsikiliza ni mwanasiasa kwenye kampeni au ni serikali kazini. Bahati nzuri wao CCM wanajua sana kuitumia mbinu hii kwani kwa kadiri ya kwamba haikatazwi kisheria basi hapa wapinzani hawana majibu imependekezwa Mawaziri wasiwe wa Bunge na ingekuwa vizuri kuwa wakati wa kampeni Waziri wa serikali asishiriki kampeni za kisiasa.

Siasa ni mikakati na mikakati ni siasa Kama alivyoonesha Msekwa katika makala yake ile naamini kuwa vyovyote vile ilivyo huwezi kumshinda mwanasiasa anayejua mikakati ya kisiasa na mbinu za kisiasa. Kuzomea kiongozi mtu mzima si mkakati mzuri wa kisiasa. Kutaja baadhi ya wanasiasa ambao wananchi wanawaona nao ni wapiganaji kwenye vita dhidi ya ufisadi si mkakati mzuri wa kisiasa hasa pale ambapo siku chache baadaye mmojawao anapata ajali!



Mkakati wa kisiasa unahitaji utaalamu. Hadi hivi sasa siamini kama Chadema au chama kingine cha upinzani kina wataalamu wa mikakati ya kisiasa (political strategists) ambao wanaweza kuwa na sauti ya kupanga mkakati wa ushindi. Siyo kila mpango wa kampeni ni mkakati wa ushindi. Mkakati hupangwa kisayansi na hutekelezwa kitaalamu kama kumfanyia mgonjwa upasuaji. Siyo kubahatisha au kupinga vidole kuombea muujiza. CCM katika hili wana wataalamu wa kutosha kabisa na wengi wanaandaliwa kwa ajili ya 2010.

Ni kwa sababu hiyo basi CCM inaposhinda tutambue kuwa kwanza siyo rahisi kuishinda lakini zaidi ya yote kwa mkakati mzuri na utekelezaji mzuri wa mkakati huo CCM inaweza kuangushwa kiurahisi tu. Lakini hili linahitaji watu wanaoweza kukaa chini kusikiliza.

Vinginevyo yale maneno ya "Kidumu chama Mapinduzi" yanaelekea kuwa na ukweli zaidi leo hii kuliko tunavyofikiria.

Soma bure

na hivyo wakati wao wanataka kupambana na wanasiasa wanajikuta wanapambana na serikali na wakati mwingine nguvu nzima ya serikali.

Fikiria Waziri wa Mambo ya Ndani (jeshi linalosimamia Polisi na wafungwa na uhamiaji) Bw. Lawrence Masha ambaye pia ni Mbunge wa Nyamagana mjini Mwanza anapokuja Busanda na kuna mamia ya Polisi maeneo hayo anaposimama kuzungumza na afande mmoja anafanya hivyo kama mwanasiasa tu kwenye kampeni, Waziri kazini au mmoja wa wakazi tu wa mji wa Mwanza? Mpinzani hapo anatoa majibu gani?

Hivyo, kwa kadiri sheria ilivyo sasa ambapo mawaziri wa serikali iliyoko madarakani wanashiriki katika kampeni katika nyadhifa zao (japo wanaweza wasiseme hivyo) ni vigumu sana kwa mpinzani yoyote kushinda kiurahisi kwani inabidi ashindane na mwanasiasa masha na wakati huo huo ashindane na Waziri Masha!

Ni kwa sababu hii wakati mwingine

MWAKYEMBE AWAJIA JUU POLISI

siana na ajali hiyo kwa madai kwamba sina utaalamu na masuala ya ajali."

Kwa mujibu wa Dr. Mwakyembe, Polisi wamefanya makosa kadhaa katika kufuatilia kesi hiyo na hivyo kumsababishia maswali zaidi. Baadhi ya makosa hayo ni pamoja na "hatua ya Polisi kuunda "Kamati Maalum" ya kupitia maelezo ya ushahidi niliyotoa na yale ya dereva wangu na kukusanya ushahidi wa ziada na baadaye kutoa uamuzi (nje ya mchakato wa kimahakama) kuwa ushahidi wangu na wa dereva wangu haukuwa sahihi, ni ukiukwaji wa mgawanyo wa madaraka wa vyombo vya dola au kwa maneno mengine ni uingiliaji wa mamlaka ya Mahakama kinyume na Katiba ya Nchi."

Zaidi ya yote kitendo cha Polisi kumuita dereva wake kuwa ni mzembe na ndiye chanzo cha ajali ni sawa na kutoa hukumu tayari baada ya wao kukusanya ushahidi wakati kazi hiyo inatakiwa kufanywa na mahakama. "Kamati hiyo imemhukumu mapema (pre-judged) kuwa mwongo na mzembe hivyo afunguliwe mashtaka mahakamani, hauendani na utawala wa sheria na misingi ya haki inayolindwa na Katiba na unaigeuza Mahakama kuwa chombo cha kupiga muhuri (rubber-stamp) maamuzi ya Polisi." Amedai Mwakyembe.

Zaidi ya yote amekanusha vikali kuwa wakati ajali inatokea alikuwa amelala (usingizi). Katika maelezo yake marefu ya kupinga ripoti ya Polisi Dr. Mwakyembe ameshangazwa ni jinsi gani timu ya wataalamu wa Polisi wameweza kufikia hitimisho kuwa alikuwa amelala wakati yeye mwenyewe anajua alikuwa macho wakati wote wa tukio?

"Nasisitiza kuwa nimeshuhudia kila kitu mimi mwenyewe hadi nilipogongwa na kitu fulani kichwani na kupoteza fahamu." Amesema Dr. Mwakyembe huku akiongeza kuwa "Kamati hiyo Maalum inadai kwamba nilikuwa nimelala ati kwa sababu ningekuwa macho ningeliumia zaidi na kwamba walikuta kiti changu kimelazwa!"

Huku akiikejeli kazi ya kamati hiyo na kuibeza, Dr. Mwakyembe ameendelea kusema kuwa "Ningetegemea madai hafifu kama hayo kutolewa na mganga wa kienyeji anayetumia ramli kufanya maamuzi na siyo Jeshi la Polisi lenye utaalamu stahili"

Zaidi ya yote amewashangaa kudai kuwa alikuwa amelala wakati ilikuwa ni saa moja tu toka atoke Makambako ambako usiku kabla yake walilala hapo. "hivyo nisingeweza kuanza kusinzia baada ya safari ya karibu saa moja tu kutoka Makambaku hadi Ifunda na kwenye mazingira ya baridi kali ya mwezi wa tano nyakati za ahsubuhi" amesema.

Akielezea ni kwa jinsi gani kitu chake kilikutwa kimeelemea kama mtu alikuwa amelalia Dr. Mwakyembe amesema kuwa "gari lilipopinduka, kiti changu kiling'oka na kunifunika kwa mbele. Hivyo nilitolewa sehemu hiyo kwa kukiiuna kiti hicho na kukilaza, jambo ambalo kwa Kamati hiyo maalum ulikuwa "ushahidi wa kitaalam" wa mimi kulala wakati wa ajali!"

Akihitimisha taarifa yake kwa waandishi wa habari Mwakyembe amesema kuwa "purukushani hizi za Polisi za "funika kombe mwanaharamu apite", zinanifanya niingiwe na wasiwasi kuwa ajali yangu haikuwa ya kawaida."

Unaweza kujisomea taarifa kamili ya Dr. Mwakyembe kwenye mtandao wetu wa Mwanakijiji.com

DA:JESSY— KUJIANDAA KWA NDOA— 2

Na. Jessica Fundi



Katika makala yangu ya mwisho wiki mbili zilizopita nilianza kuzungumzia suala zima la maandalizi ya ndoa. Niliishia kwa kusema kuwa kuna kitu kimoja cha msingi ambacho kila mwana ndoa ni lazima ajiandae nacho kwanza kabla ya kujiandaa kwa harusi, familia, nyumba n.k

Kitu hicho ambacho niendelee nacho leo ni kitu ambacho kwa wengine ni kidogo lakini ndicho kinaweka msingi mkubwa sana wa maisha ya ndoa huko mbeleni; nacho ni kubadili mawazo kutoka maisha ya ukapera kwenda kuwa na mwenza.

Inachukua muda mrefu kidogo kwa mtu kuweza kubadili matendo yake hadi ukakubaliana na ukweli kuwa sasa hivi mtu huyo si kapera tena.

Kama ni mwanamme ni lazima atambue kuwa anapoingia kwenye ndoa maana yake ni kuwa mwanamke wa kwanza kumjali, kumlinda, kumfurahisha na kumtuza ni mkewe na si yule dada kazini au yule abiria mwingine ndani ya basi.

Vile vile kwa kina dada ni lazima kutambua kwanza kabisa kuwa mwanamme pekee ambaye anatakiwa umpendezeshe, umfanye ajisikie anapendwa na kuonesha kuwa unamjali ni mumeo.

Maana ya hili ni kuwa, unapomchukulia mwenzi wako kama mmoja wa "wanaume" au "wanawake" wengine unajiandaa kuidhoofisha ndoa yako kwani endapo atatokea mwanamke mwingine akamuonesha kile anachokikosa nyumbani, kumjali, kumchekesha, kujishaua (flirting) na kumpa penzi la nguvu basi usishangae ukawa unalala usiku peke yako.

Vivyo hivyo kwa wanaume; endapo mke wako unamtendea kama kina Hadija, Jenny na Mwajuma, akatokea mwanamme mwingine akamuonesha kumjali, kumfurahisha, kumsikiliza na kumpa penzi la nguvu, usije ukashangaa unarudi nyumbani na jikoni kuna baridi tu!

Hayo yote yanaweza kuepukwa kwa kujiandaa kiakili pale uamuzi wa ndoa unapochukuliwa. Kutambua kuwa huyo ninayetaka kumchumbia ndiyo atakuwa kwangu nuru, taa, na nyota yangu. Atakuwa ndiyo furaha yangu, rafiki yangu na zaidi kabisa mwenzi wa maisha yangu.

Kushindwa kulipokea wazo hilo, kulikubali na kulikumbatia kwa furaha kunafanya ndoa ijengwe kwenye msingi wa "liwalo na liwe". Tutaendelea wiki ijayo:
Niandikie: **dajessy@klhnews.com**

Soma Bure
hoja zenye nguvu

RIWAYA ZA MWANAKIJIJI ZUWENA: BINTI WA KITANGA – 4

(kutoka toleo lililopita)
Moyo uliniuma nilishindwa kujizuia nikaanza kulia kama mtoto mdogo. Nilimsogelea Zuwena, na nilikiri pendo langu kwake milele na jinsi binti huyo wa kitanga alivyobadilisha maisha yangu. Niliendelea kubwabwaja kwa uchungu mkubwa.

"Zuwena Nakupenda sana na nitaendelea kukupenda" Nilimwambia.

Ghafla Zuwena alifumbua macho yake. Nikasogea karibu yake zaidi kusikia.

Na yeye akaninong'oneza kitu. Na baada ya kusema alichosema alifumba macho na kuvuta pumzi yake ya mwisho huko mashine zikianza kulia kuonyesha kuwa moyo wake umeanza kuacha mapigo. Niliwaita manesi kwa sauti kubwa iliyojaa hofu na mashaka. Waliijitahidi kujaribu kumrudisha lakini juhudi zao zilikuwa ni za ukomo wa mwanadamu.

Daktari aliniuliza kama niko tayari kuwapa ruhusa wamfanyie upasuaji wa C-Section ili wajaribu kumtoa mtoto hai kwani alikuwa ameshafikia miezi karibu tisa. Niliwapa ruhusa bila kujua hasa ni nini nitafanya.

Walimuweka kwenye vyombo vya kisasa vya kusukuma damu mwilini wakati upasuaji wa kumtoa mtoto ukifanyika.

Muda si mrefu baadaye mtoto wa kiume alizaliwa, siku ile ile ile mama yake anafariki. Wakati huo wazazi wa Zuwena na wenyewe ndiyo walikuwa wamefika tu pale. Wakawa wanajaribu kunisogelea kuniuliza kulikoni na kunipa pole. Sikuweza; nilishikwa na donge la roho.

Niliamka na bila hata ya kuwasalimia niliondoka hospitali ya Bombo huku nikilia na hasira ikiwa imenipanda kichwani. Niliingia ndani ya gari langu Peagout 504 Pick UP mali ya Mamlaka ya Mkonge na kuanza kukanyaga mafuta.

Kama vile ilikuwa siku ya uchuro radio Tanzania walianza kupiga wimbo ule wa wana OSS wakiwa chini ya Marijani Bin Rajab lakini ukiwa ni marudio ya Mtoto wa Dandu: "Zuwena, mtoto aliyeumbika".

* * *

Baada ya mazishi, wazazi wa Zuwena walinikaribisha katika jitihada za kunipatanisha nao. Waliniomba radhi kwa kila namna. Sikuweza kusema lolote wakati ule. Nilimchukua mtoto wangu kulelewa na mama yangu na dada yangu mkubwa. Sijui kama atakuja kuujua ule upande wa familia yake. - **MWISHO**

NGUVU YA HOJA:TUSUSIE BIASHARA ZA MAFISADI

Allien (JamiiForums.com)

Kwa Nini?
Kwa kuwa Serikali na Vyombo vya Dola vimeshindwa kuwashughulikia mafisadi na Kuwachukulia hatua kali stahiki. Hukuna tena mtu wa kutusaidia. Tumepiga kelele hakuna anyetusikia. Tumelia bado wazeziba masikio. Ndugu zetu wamekufa hakuna anayetuonea huruma.

Wanachofanya Mafisadi:
Mafisadi ni watu wanaotumia rasilimali za taifa kwa manufaa yao binafsi. Aidha hutumia madaraka yao vibaya kwa kujinufaisha ama hutumia njia za udanganyifu kuiba pesa za umma kwa manufaa yao binafsi.

Madhara yanayoletwa na Mafisadi:
Wengi wamepoteza maisha yao kwa sababu ya Ufisadi. Kuna ambao wameathikika ama moja kwa moja ama kupitia sababu ambayo imesababishwa au kuchangiwa na ufisadi.

Nini cha Kufanya:
Inabidi sasa tujipange vema kupinga ufisadi kwani tumeachwa kama watoto yatima ambao wazazi wao walishafariki na kuchukuliwa na mlezi ambaye pia amekabidhiwa mali ya watoto lakini akaanza kujinufaisha yeye na nafsi yake.

Kwa namna gani?
Kwa kususia bidhaa na huduma zote zinazotolewa na makampuni yanayomilikiwa na mafisadi hata kama ina maana kwa kufanya hivyo tutaabika. Hii itawafanya watambue kuwa sasa imefika mahali hatukubali tena. Hii pia itasaidia kuvunja vunja nguvu zao za kifisadi na kiuchumi kwa kiasi fulani.

Nini tena?
Tubuni na mikakati mingine ambayo pia itasaidia kuhakikisha mafisadi wote wanadhibitiwa kwa nguvu ya umma.

Tushiriki Vipi?
Kwanza kila Mwana JF asign katika thread hii na kuonyesha kiasi gani anunchukia UFISADI. Kisha ashiriki kwa vitendo katika kususia bidhaa na huduma zote zinazotolewa na makampuni yanayomilikiwa na mafisadi.

Nitajuaje Huduma na Bidhaa Zao?
Kila asomaye hapa na aandike kwa Uhakika Makampuni yote Yanayomilikiwa na Mafisadi kwa Majina na Kutaja wamiliki wake na Ufisadi Uliofanywa.

Baada ya Hapo?
Sambaza Waraka huu kupitia barua pepe na njia nyingine zote zinazoweza kufanikisha kufikisha ujumbe huu kwa Wananchi Wote wa Tanzania.

Kampeni Inaanza Lini?

Natoa Mwito Kampeni hii ianze Tarehe 01-06-2009

Mhariri:
Je hili wazo linatekelezeka? Itakuwaje kama biashara za mafisadi ndizo tunazozitegemea kila siku?

TUNATAFUTA WAANDISHI

Tuma: **mhariri@klhnews.com**

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

KATUNI ZA WIKI

Picha ya Wiki



Mara baada ya ajali Dr. Harrison Mwakyembe akipelekwa hospitali.





PATA HABARI MOTOMOTO NA MIJADALA

http://www.mwanakijiji.com

Jiandikishe kushiriki mijadala, kupata habari, kusikiliza muziki masaa 24 na matangazo ya moja kwa moja kila mwishoni mwa juma.

Ukizungumzia habari, unatuzungumzia

KUTOKA KWENYE MTANDAO

Nyie andikeni mnavyotaka, hata kwenye TV onyesheni, kwanza watu wa huku TV hawana kwa vile hata umeme hawana! Hizo TV zenu watazitazamia wapi.

Na nyine wenye magazeti kwanza huku hayafiki na hata yakifika wananchi hawana uwezo wa kuyanunua, watasomea wapi hizo fitina zenu. Hayo mnayoandika yanabakia kuwa yenu na wamiliki wa vyombo vyenu—**Mkuchika**

Hwana umeme, kwa nini? Magazet hayafiki, kwa nini? Hawana uwezo wa kununua magazeti, kwa nini? Nani kawaweka wananchi katika haya mazingira hata hawawezi kuwa na TV, Umeme wala kusoma gazeti? Kwani aliyesababisha haya yote hajulikani? - **Mama Mdogo**

Hivi, mbona kamati ya Ulinzi na Usalama wa Taifa haijamfuata Chenge, Karamagi, Msabaha, Idrissa na hata Mwakyembe na Rostam na kuwahoji kuhusu tuhuma za Ufisadi zilizo juu ya vichwa vyao?

Kwa nini Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Taifa haijafanyia kazi mapendekezo ya Ripoti ya Warioba au Ripoti ya Amina Chifupa ya wenye kufanya biashara za kulevya? - **Rev. Kishoka**

Mathalan, nyumba yangu imeungua moto. Kwa mantiki ya kamati hiyo maalum, siruhusiwi kuelezea kuwa chanzo cha moto kilikuwa kibatali au mshumaa, mpaka nimsubiri Kombe na timu yake ya "wataalam" waje kupiga ramli kama walivyofanya kwenye ajali yangu? - **Dr. Mwakyembe**

Kujenga nchi si lazima kila mtu ajazane Dar, kwani siku hizi kunama global economy, mtu anaweza kusunda mshiko mzuri na kutuma remmittance bongo.Sio lazima wote turudi, uchumi wenyewe mdogo hata tukitaka kuanzisha biashara purchasing power ya kuridhisha wote haipo.— **Blueray**

TOA NAKALA MOJA

Cheche za Fikra
Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie:
mhariri@ klhnews.com

Tovuti: http://www.mwanakijiji.com

***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*